Aghalabu, inategemewa mteja atakuwa pia ndiye mtumiaji, lakini kufuatana na tafsiri zilizotangulia, inawezekana kabisa kwamba mteja asiwe mtumiaji na mtumiaji asiwe mteja. Kwa mfano, mtu akinunua simu kwa ajili ya matumizi ya ofisi na kuiunganisha na mtandao wa simu kwa kuisajili laini kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa, aliyenunua na kusajili laini ndiye mteja wa kampuni husika. Mtumiaji anaweza kuwa mtu mwingine kabisa. Hivyo hivyo kwa kutumia mfano wa televisheni/runinga, mmiliki au mwendeshaaji wa hoteli anaponunua televisheni/ luninga na kujiunga na huduma ya shitariki anakuwa mteja wa kampuni husika ya utangazaji; lakini watumiaji wa televisheni/runinga hizo ikiwa ni pamoja na maudhui ni watu wengine.



Pamoja na maelezo hayo, hii haizuii ama kwa mteja au kwa mtumiaji kutopata haki zake kisheria na kwa mujibu wa kanuni zinazosimamia sekta ya mawasiliano.

3.0 Sekta ya Mawasiliano Tanzania

Sekta ya mawasiliano nchini inahusisha miundombinu, utoaji na matumizi ya huduma na bidhaa katika sekta ndogo za simu na intaneti, utangazaji, posta na usafirishaji wa vipeto.

Huduma za Mawasiliano ni za msingi katika maisha ya wananchi kijamii, kiuchumi na kisiasa. Mawasiliano yanawezesha na kuhimili sekta nyingine.

Watoa huduma za mawasiliano wanapewa leseni na kusimamiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

4.0 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania au TCRA ambacho ni kifupisho cha Tanzania Communications Regulatory Authority kwa lugha ya kiingereza ni taasisi ya serikali inayosimamia sekta ya mawasiliano katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. TCRA inasimamia sekta ndogo za mawasiliano ya simu, intaneti, maudhui ya utangazaji (redio na televisheni) na huduma za posta na usafirishaji wa vipeto. Mamlaka inasimamia maudhui kwa Tanzania Bara tu. Zanzibar ina tume inayosimamia maudhui ya utangazaji kwa eneo la Zanzibar. TCRA ilianzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ya 2003.

TCRA imeweka mfumo wa leseni wenye lengo la kuendeleza maeneo ya sekta ndogo zilizotajwa hapo awali. Leseni zinazotolewa ni pamoja na Leseni ya kumiliki na kuweka muundombinu; Leseni ya Mawasiliano; Leseni ya kutoa huduma za

Mawasiliano, Leseni ya kutumia masafa na namba na Leseni za Maudhui kwa ajili ya redio na televisheni.

Mamlaka pia inatoa leseni za kusambaza na kusafirisha barua na vifurushi, kufunga na kutengeneza vifaa; Leseni ya kuingiza nchini na kusambaza vifaa vya mawasiliano; Leseni ya kuuza vifaa vya mawasiliano vya jumla, Leseni ya kuuza vifaa vya mawasiliano kwa rejareja na Leseni ya kufunga au kuweka mitambo ya mawasiliano.

5.0. Wadau wa Sekta ya Mawasiliano Tanzania


Sekta ya mawasiliano Tanzania ina wadau wakuu wanne ambao ni Serikali, Watoa huduma, Watumiaji wa huduma na TCRA ambaye ni msimamizi wa sekta. Wadau hawa wana majukumu, matarajio na malengo tofauti kama inavyoainishwa hapo chini: -

Serikali-inatunga sera, sheria na kanuni zinazoongoza sekta pamoja na kukusanya kodi zinazotokana na shughuli za sekta kwa maendeleo ya nchi na watu wake.

Watoa huduma-wanafanya biashara, wamejipanga vizuri, wanahamasishwa na kupata faida, wana uwezo (nguvu ya fedha).

Watumiaji-hawajajipanga, wanatazamia kupata huduma bora kwa gharama kidogo au ikiwezekana hata bure, hawana umoja na wengi wana ufahamu mdogo kuhusu teknolojia ya mawasiliano pamoja na huduma wanazozitumia.

Mdhibiti/Msimamizi (TCRA) - yuko katikati ya wadau hawa wengine ili kuhakikisha mahitaji na matazamia yao yanafikiwa kwa kuzingatia uwiano sawia wa manufaa katika sekta ya mawasiliano. Mamlaka inatekeleza sera za Serikali, inahakikisha sekta haiyumbi kwa kuhakikisha watoa huduma wanatoa huduma kwa ufanisi na kuona maslahi ya watumiaji yanalindwa.



6.0 Kazi na Majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Sheria iliyoanzisha Mamlaka hii imetamka kazi za TCRA kama zinavyoainishwa hapa chini: -

1. Kutoa leseni, kuongeza muda wa leseni na kufuta leseni pale ambapo masharti ya leseni husika hayaku-fuatwa;
2. Kuweka viwango kwa bidhaa na huduma zinazosimamiwa;
3. Kuweka viwango, kanuni na masharti ya kusambaza bidhaa na huduma zinazosimamiwa;
4. Kudhibiti viwango na bei ya jumla ya mawasiliano kati ya mitandao;
5. Kufuatilia utendaji wa sekta zinazosimamiwa kuhusiana na: -
 - a. Viwango vya uwekezaji, upatikanaji wa huduma, ubora na viwango vya huduma, gharama za huduma, ufanisi wa bidhaa na usambazaji wa huduma;
 - b. Kuwezesha kutatuliwa kwa malalamiko na mtigogoro baina ya watoa huduma na kati ya mtoa huduma na mtumiaji wa huduma;
 - c. Kusambaza taarifa kuhusu mambo ambayo ni muhimu kwa ajili ya shughuli za Mamlaka.

Katika kufanya kazi zake, Mamlaka inajitahidi kuendeleza ustawi wa jamii ya Tanzania kwa kukuza ushindani unaofaa na ufanisi wa uchumi; kulinda maslahi ya watumiaji; kuendeleza upatikanaji wa huduma zilizodhibitiwa kwa watumiaji wote ikiwa ni pamoja na wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji walio katika mazingira magumu;

kuelimisha wananchi kuhusu utambuzi na uelewa wa sekta zilizodhibitiwa ikiwa ni pamoja na haki na wajibu wa watumiaji na namna ambavyo malalamiko yanaweza kuwasilishwa na kutatuliwa.

7.0. TCRA na dhana ya kumlinda Mtumiaji

Sekta ya mawasiliano inakua na kubadilika wa kasi. Kuna huduma na bidhaa nyingi ambazo zinavutia watumiaji tofauti-tofauti kutokana na hadhi yao, kiwango cha uchumi, uelewa na mahali walipo. Wateja na watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano wakiwa wadau muhimu katika sekta ya mawasiliano wanahitaji kulindwa dhidi ya watoa huduma ambao wanaweza kutumia udhaifu w a watumiaji au uelewa wao mdogo kuwakandamiza, kuwanyonya, kuwadhihaki na kuwanyanyasa kiuchumi.

TCRA inapotoa leseni huweka masharti ambayo hulenga kumlinda mtumiaji. Uwekaji wa viwango kwa bidhaa na huduma zinazosimamiwa una lengo la kuhakikisha kwamba watumiaji wanapata thamani ya malipo waliyotoa kwa huduma na bidhaa. Viwango na kanuni na

masharti ya kusambaza bidhaa na huduma zinazodhibitiwa vinawekwa kwa madhumuni ya kuendeleza biashara inayozingatia ubora wenye viwango vya kimataifa na vitakavyo hakikisha watumiaji wanapata huduma kwa viwango stahiki. Udhibiti wa gharama na bei za huduma una lengo la kuzuia mtoa huduma mwenye ukiritimba kuwanyonya watumiaji kwa kujipangia bei anayotaka kwa kutumia fursa ya kutokuwepo ushindani.

Majukumu ya kushughulikia malalamiko ya watumiaji yana lengo la kuhakikisha kwamba watumiaji wanatendewa haki na kwa muda mfupi iwezekanavyo ikilinganishwa na muda ambao ungehitajika kwenye vyombo vingine vya kutoa haki.

Aidha, Mamlaka inapohimiza kuenea kwa huduma vijijini na kwenye maeneo ambayo watoa huduma wasingependelea kwenda kwa sababu za kibiashara, hufanya hivyo kwa lengo la kuhakikisha kwamba Watanzania wengi zaidi wanapata huduma, bila kutengwa kwa sababu ya eneo wanaloishi.

8.0. Haki za Watumiaji

Watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano wana haki mbalimbali ambazo zinawapa ulinzi wanapotumia huduma na bidhaa hizo. Haki hizi, ambazo zimeainishwa kwenye Kanuni za Kulinda Watumiaji, zinatokana ama na matumizi ya huduma au bidhaa husika, masharti ya leseni za watoa huduma au kwa mujibu wa matakwa ya sheria za nchi.

8.1. Haki zitokanazo na matumizi na masharti ya leseni

Upatikanaji wa huduma: Watumiaji wanapaswa kupata huduma za msingi za mawasiliano kwa bei nafuu.

Kupata huduma bora: Watumiaji wanatakiwa kupata huduma zenye ubora ambazo zinaendana na gharama za huduma. Wanapaswa kupata huduma ambazo zinaendana na dhana ya thamani ya fedha inayolingana na huduma zinazotolewa.

Kupewa taarifa kuhusu huduma na bidhaa: Watumiaji wana haki ya kupata taarifa kamili za makubaliano ya awali ambazo ziko wazi (zinaeleweka), zitakazosaidia, zinazojitosheleza na sahihi kuhusu huduma zinazotolewa na mtoa huduma ili kurahisisha kufanya uchaguzi sahihi.

Kutokubaguliwa: Watumiaji wana haki ya kuhudumiwa kwa usawa na bila kubaguliwa. Ubaguzi unaozungumziwa hapa unaweza ukawa kwa namna ya ama kunyimwa huduma au huduma kutolewa kwa ubora



usiofanana kwa wateja tofauti hata kama wote wanalipa kiasi cha fedha sawa na wengine na kwa huduma zinazofanana.

Malalamiko: Watumiaji wanapokutana na kasoro katika ubora wa huduma au ucheleweshaji katika kupata huduma wanatakiwa kulalamika. Watumiaji wanatarajiwa kutumia huduma wakijua masharti na viwango vya huduma inayotolewa. Kama masharti hayo hayakutumizwa mtumiaji anatakiwa kulalamika.

Kutatuliwa matatizo: Mtumiaji anapolalamika anatakiwa apate suluhisho la matatizo yake. Kila mtoa huduma anatakiwa kuweka utaratibu wa kutatua malalamiko ya wateja kuhusiana na huduma anazozitoa au matatizo yanayotokana na huduma hizo.

Iwapo mtoa huduma ama hakutatua tatizo au hakulishughulikia kabisa au utatuzi uliotolewa haukumridhisha mlalamikaji basi mlalamikaji anatakiwa kuwasilisha malalamiko yake TCRA.

Kupewa taarifa kabla ya kusimamisha au kukatisha huduma: Iwapo kwa namna moja au nyingine mtoa huduma anataka kusimamisha kwa muda utoaji wa huduma anatakiwa kutoa taarifa ya awali kwa watumiaji akieleza wazi sababu za kufanya hivyo. Kusitishiwa huduma bila kupewa taarifa ni ukiukwaji wa haki za watumiaji.

Uwakilishi: Watumiaji wana haki ya kuwakilishwa katika kufuatilia masuala ya huduma wanazopata.

Kupata taarifa kamili za malipo na ankara: Watumiaji wanaolipia huduma baada ya kutumia, wana haki ya kupata taarifa kuhusu ankara zao kwa ajili ya malipo wanayotakiwa kufanya.

8.2. Haki zinazotokana na Sheria za nchi

Zipo haki ambazo zimewekwa kwenye sheria; nazo ni usalama wa huduma zinazotolewa, usiri na faragha wakati wa matumizi na elimu kuhusu huduma zinazotolewa. Haki hizo ni:

Usalama na Ulinzi: Watumiaji wanatarajia kutumia huduma na bidhaa ambazo ni salama na imara. Mtoa huduma, muagizaji au msambazaji wa vifaa vya mawasiliano hapa nchini, anapaswa kuhakikisha kwamba vifaa vyake vyote vinakidhi mahitaji ya usalama wa afya kabla ya kutumiwa na wateja. Vifaa vya mawasiliano vinavyoingizwa Tanzania vinatakiwa kuthibitishwa ubora wake na TCRA, kuwa salama kwa watumiaji kwa kuzingatia viwango vya ubora wa kimataifa.

Kuwa na usiri au faragha katika matumizi: Sheria inamlinda mtumiaji dhidi ya kutolewa kwa taarifa zake na mtoa huduma kwa watu wasiohusika. Watumiaji wana haki ya usiri au faragha katika matumizi ya huduma. Sheria imeweka masharti ya uaminifu kwa watoa huduma ili kuhakikisha na kudumisha usiri wa maudhui ya mawasiliano yote, ziwe data au taarifa zozote ambazo mtoa huduma anaweza kuvipata kutokana na kumhudumia mteja. Taarifa za mteja hazitatolewa kwa mtu yeyote bila ya ridhaa ya maandishi ya mteja mwenyewe.

Taarifa zinaweza kutolewa kwa wahusika walioidhinishwa pale tu ambapo zinahitajika katika uchunguzi wa matukio ya kijinai na kwa utaratibu uliowekwa kisheria na kikanuni au itakapoombwa na mahakama.

Elimu kwa Watumiaji: Watumiaji wana haki ya kuelimishwa kuhusu huduma wanazotarajia kujiunga nazo na zile zinazotolewa kwao na masuala yanayohusiana na matumizi yao.

9.0. Wajibu wa watumiaji

Pamoja na haki walizonazo, watumiaji pia wana wajibu ambao wakati mwingine unafanana na haki. Wajibu unatokana na matumizi pia na sheria za nchi.

9.1 Wajibu kutokana na matumizi

Kuwa makini: Ni jukumu la mtumiaji kuwa makini na kuhoji masuala kama vile kanuni na masharti ya huduma. Wateja wanapaswa kujua haki na wajibu wao pamoja na kutafiti taarifa nyingine wanazoweza kupata ambazo zinahusiana na huduma ambazo wanazitumia au wanatarajia kuitumia. Aidha watumiaji wanatakiwa kujilinda dhidi ya makosa yote ya mtandaoni, ikiwemo ulaghai na uhalifu unaofanywa kwenye mtandao ya mawasiliano.

Kuunga mkono udhibiti: Watumiaji wanatakiwa kutoa taarifa TCRA pale ambapo wanaona kasoro katika utoaji wa huduma yoyote katika matumizi ya huduma za mawasiliano.

Kutokubughudhi watumiaji wengine: Kila Mtumiaji anapaswa kutumia huduma na bidhaa za mawasiliano kwa staha, bila ya kuwaletwa kero watumiaji wengine. Hii ni pamoja na kuzingatia faragha ya watu wengine kwa mfano kwenye sehemu za ibada; sehemu zinazohitaji umakini kwa mfano maktaba, benki na kwenye mikusanyiko ya watu wengi. Katika wajibu huu, inasisitizwa kwa mtumiaji kutotuma ujumbe, au kupiga simu zenye maudhui isivyo stahiki kwa mtumiaji mwingine bila ridhaa yake.



9.2. Wajibu unaotokana na Sheria za nchi

Kutii sheria za nchi: Mtumiaji ana wajibu wa kutumia huduma kwa kuzingatia sheria za nchi na bila kuingilia uhuru na haki za watumiaji wengine. Huduma za mawasiliano zisitumike kama nyenzo ya kufanya uhalifu wa aina yoyote; mfano kutukana watumiaji wengine, kutunza au kusambaza picha zisizofaa, kufanya mawasiliano yenye maudhui ya kulenga ponografia ikiwemo ponografia inayohusu watoto. Sheria mojawapo ni sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta (EPOCA) ya 2010, Sheria ya makosa ya Mtandao ya 2015 na Sheria ya Miamala ya Kielektroniki ya 2015.

Baadhi ya matakwa ya kisheria kuhusu matumizi ya huduma za mawasiliano ni pamoja na kusajili laini ya simu kwa majina halisi kabla ya kuanza kuitumia, kutoa taarifa unapoteza simu au laini ya simu au unapobadilisha umiliki wa simu. Kuchakachua laini ya simu au kifaa chochote cha mawasiliano ni kutenda kosa la jinai.

Matumizi halali ya huduma: Watumiaji wanatakiwa kutumia huduma kwa kuzingatia masharti ya huduma husika. Matumizi ya huduma kinyume na malengo yaliyowekwa ni kukiuka sheria za nchi.

Matumizi salama ya huduma: Watumiaji wa huduma na vifaa vya mawasiliano wanatakiwa kutumia huduma na vifaa vya mawasiliano kwa usalama wao binafsi na watumiaji wengine na pia kuhakikisha utunzaji wa mazingira. Watumiaji wanatakiwa kuzingatia maelekezo kuhusu matumizi ya simu zao za kiganjani wanapokuwa kwenye maeneo hatarishi au maeneo maalum kama vituo vya mafuta, hospitali (karibu na vifaa tiba ambavyo vinaweza kuathiriwa ubora wa utendaji wake kwa kuingiliwa na matumizi ya simu) au wanapoendesha magari. Watumiaji wachukue tahadhari na wazingatie maelekezo yanayotolewa kwenye maeneo husika.

Kulipia huduma wanazotumia: Watumiaji wanawajibika kulipa gharama za huduma ambazo wamejiunga nazo, hasa kwa wale wanaolipia huduma baada ya matumizi. Kwa wale wanaolipia kabla, ni vyema kufahamu huduma wanazotumia na gharama zake. Mamlaka inawashauri watumiaji kujiunga na vifurushi ikiwa vipo kwani gharama zake ni ndogo kuliko bei ya kawaida. Kujiunga na vifurushi ni hiari ya mtumiaji mwenyewe.

Kuhifadhi Mazingira na Utunzaji wa nyenzo za mawasiliano: Kila mtumiaji ana jukumu la kuhakikisha kuwa matumizi yake ya huduma za mawasiliano hayaathiri mazingira. Aidha mtumiaji ana jukumu la kutunza vifaa, miun-

dombinu na nyenzo zote za mawasiliano karibu yake.

10.0. Masuala ya kuzingatia unaponunua na kutumia huduma za mawasiliano

Unaponunua kifaa cha mawasiliano au huduma za mawasiliano unakuwa na matarajio mengi. Kwanza ungependa kifaa au huduma ikidhi mahitaji yako na uridhishwe na ubora wake, ufanisi na upatikanaji wa huduma muhimu zitakazofanya uweze kuendelea kufaidi na kuifurahia bidhaa au huduma husika. Ungependa pia kupata msaada au kuungwa mkono na aliyekuuzia au anayekupa huduma ili uweze kuendelea kutumia huduma na bidhaa hiyo kama ulivyotarajia mwanzoni. Hivyo, kuna mambo ambayo ni muhimu kuzingatia, ambayo yameainishwa hapa kutegemea na aina ya huduma au kifaa.

10.1. Unaponunua simu

Simu imekuwa kifaa ambacho kina matumizi mengi ya mawasiliano. Simu ya mezani inafanikisha mazungumzo na baadhi huweza kutoa huduma za ujumbe mfupi (sms) na huduma za intaneti. Simu ya kiganjani inatumika kwa mazungumzo, kutuma ujumbe mfupi, kupata huduma za intaneti, kufanya miamala ya kifedha, kujumuika kupitia mitandao ya kijamii na hata kuhifadhi kumbukumbu, kutegemea uwezo wa simu husika. Simu ni nyenzo ya kutunganisha kibiashara na kijamii; hivyo mnunuzi wa simu angependa kuwa na kifaa ambacho kinakidhi mahitaji na matarajio yake kutegemea na kile anachotaka kufanya.

Iwapo mahitaji yako ni mazungumzo na kutuma ujumbe mfupi au kupata huduma za kifedha tu, simu ya kawaida inakufaa. Iwapo una matumizi na matarajio zaidi ya kuzungumza na kutuma ujumbe mfupi, unahitaji kuwa na simu yenye uwezo wa kufanya mambo unayotarajia.

Pamoja na mahitaji haya ya mawasiliano, unahitaji kuwa na simu ambayo itakuwezesha kuitumia wakati wote. Hivyo, pamoja na mazingatio ya mahitaji yako ya matumizi, unahitaji simu yenye sifa zifuatazo:

1. Ubora: Kabla ya kununua simu, uhakikishe uhalisia na ubora wake kwa kuangalia namba tambulishi ya simu husika. Kila simu halali ya kiganjani ina namba yake ya pekee ya utambulisho ambayo inajulikana kama IMEI, ambacho ni kifupisho cha maneno ya kiingereza ambayo ni International Mobile Equipment Identity, na namba hii haifanani na nyingine yoyote duniani kote.

2. Uwezo wa kuunganisha mitandao: Hakikisha kuwa simu unayonunua inaweza kuunganishwa na mitandao iliyoko nchini na nje ya nchi pia.



3. **Urahisi wa kuchaji:** Simu iwe na uwezo wa kutumia kifaa cha kuchajia ambacho kinapatikana kirahisi.

4. **Utunzaji wa umeme:** Hakikisha simu ina uwezo wa kutunza umeme kwenye betri yake na kukupa muda wa kutosha kutumia huduma za mawasiliano, yaani ambayo ikichajwa inakaa muda mrefu bila betri kuisha nguvu.

5. **Urahisi wa kutumia:** Hakikisha unanunua simu itakayo kuwezesha kupokea simu na meseji bila kupitia mlolongo wa hatua ndefu.

6. **Simu ya kiganjani isiwe kero:** Nunua simu inayoweza kushikwa mkononi na kutumiwa bila kuleta bugudha kwa mtumiaji au kwa watu wengine.

7. **Mahali pa kununua simu:** Ni jambo la muhimu kuhakikisha unanunua simu yako mpya kutoka kwenye duka lililosajiliwa au kuidhinishwa na watoa huduma au watengenezaji wa simu husika. Hii itakuhakikishia kuwa iwapo kuna tatizo la simu uliyonunua, basi utaweza kutengenezewa simu yako iliyo kwenye waranti au wakati mwingine kubadilishiwa kabisa.

8. **Dai risiti na waranti:** Kila ununua simu mpya, hakikisha unadai risiti na waranti ambavyo vitakuhakikishia umiliki wako na pia uhakika wa yule anayekuuzia. Pale inapotokea unataka kununua simu iliyotumika, hakikisha unapata risiti ya awali au uthibitisho wa umilki wa simu husika. Simu bora inatakiwa iwe na garantii ya angalau mwaka mmoja.

9. **Pata taarifa kabla ya kufanya uamuzi:** Pamoja na vidokezo vilivyotajwa hapo juu, unaweza pia kupata simu inayokufaa kwa kusoma taarifa za kifaa chenyewe au kupata uzoefu/maoni ya watumiaji wengine ambao wameridhika na ubora, utendaji kazi wa simu husika; ila taarifa hizo zitoke kwa watu unaowaamini.

10.2. Unaponunua laini ya simu

Ili simu ya kiganjani iweze kufanya kazi, inahitaji iwe na laini ambayo imeunganishwa na mtandao husika. Laini hii inajulikana kama SIM card, ambacho ni kifupisho cha Subscriber Identity Module kwa lugha ya kiingereza.

Sheria inataka mtumiaji anayenunua au kupata laini ya simu kuisajili kwa majina yake halisi. Kwa mujibu wa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektoniki na Posta (EPOCA) ya 2010, adhabu ya kutokufanya hivyo ni shilingi 300,000 au kifungo miezi mitatu. Hakikisha taarifa unazotoa wakati wa usajili ni za kweli. Ni kosa la jinai kutoa taarifa za uongo, na inapothibitishwa mahakamani, adhabu kali hutolewa ikiwa ni pamoja na faini, kifungo au vyote viwili.

Kuthibitisha usajili wako, piga *106#.

Ni muhimu kuhakikisha kwamba kitambulisho chako ndicho kinachotumika katika usajili wa laini. Vitambulisho ambavyo vinakubalika ni:

1. Kitambulisho cha Taifa.
2. Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.
3. Pasi ya Kusafiria.
4. Kitambulisho cha Mpiga Kura.
5. Leseni ya Udereva iliyotolewa Tanzania.

Ni vyema kuchagua mtoa huduma ambaye atakidhi matarajio yako na ambaye una imani kuwa atakupata huduma bora kwa gharama unayoimudu. Ujiunge na mtoa huduma ambaye atakuwa tayari kukuhakikishia haki zako, ikiwa ni pamoja na haki ya kuwasilisha malalamiko na kupata suluhisho.

10.3. Unapojiunga na huduma za simu

Watoa huduma za simu za kiganjani wana bidhaa nyingi ambazo huweza kuunganishwa kama huduma moja (kifurushi). Kuna aina nyingi za vifurushi vyenye gharama tofauti. Unapojiunga na huduma au vifurushi, ni vyema kuzingatia aina ya huduma unayotarajia; kama ni ya mazungumzo zaidi, meseji zaidi au data zaidi.

Pata taarifa za kutosha kabla na wakati wa kutumia huduma hizo na wakati wote, pata ufafanuzi wa huduma unayojiunga nayo iwapo utakuwa huna uhakika na lile linaloendelea, hasa pale unapoonza kipengele cha 'masharti na vigezo kuzingatiwa' kinasisitizwa.

10.4. Unapotumia simu kwa maongezi au kutuma ujumbe mfupi

Matumizi ya simu kwa maongezi ni ya aina mbili – kupigia mtumiaji mwingine na kupokea simu kutoka kwa mtumiaji mwingine. Maongezi ya simu yanatakiwa yawasilishe ujumbe unaotakiwa kwa muda mfupi. Hii inaokoa muda na pia gharama za matumizi. Mawasiliano kwa njia ya ujumbe mfupi yanaokoa gharama za maongezi na pia ni nzuri kutumika kwenye hadhara, kwani ina faragha na huondoa kuwabugudhi watu wengine. Unapotumia simu kuwasiliana zingatia vidokezo hivi muhimu:

1. Fikisha kwanza ujumbe uliokufanya upige simu, ndipo uongee mambo mengine.

2. Simu nyingi zina milio ndani ya kifaa chenyewe, lakini pia mtumiaji anaweza kupata milio mingine kwa namna mbalimbali na kuihifadhi kwenye simu yake. Ni vyema kuweka mlilo wenye staha na heshima kwenye simu yako, kwa kuzingatia maadili ya hadhara/jamii inayokuzunguka.



3. Zingatia faragha yako na ya watu wengine; kwa mfanano kwa kutokupayuka unapokuwa kwenye mkusanyiko wa watu, (mfano benki, maeneo ya ibada na tafakuri, hospitali, kwenye mikutano, darasani n.k). Kwa kawaida, sauti ya mtu anapozungumza na simu inakuwa ni ya juu tofauti na mazungumzo ya ana kwa ana. Ukitaka kutumia simu kwenye hadhara, kaa mbali na watu wengine, angalau hatua nne kutoka mtu wa mwisho kwenye mkusanyiko huo au kama ni kwenye chumba, ni vyema zaidi ukitoka nje ya chumba husika.

4. Usitumie simu kwenye maeneo hatarishi ambayo yanaweza kukufanya ushahidi unachofanya; kwa mfano unapoendesha gari au mitambo, unapokuwa jikoni, unapotembea barabarani, n.k. Usitumie simu katika mazingira ambayo yanaweza kuwapa nafasi watu wenye nia mbaya kukufanyia uhalifu.

5. Zingatia masharti ya matumizi ya simu (kwa mfano ukiwa ndani ya ndege, maeneo nyeti, n.k).

6. Usipigie watu simu au kuwatumia meseji muda ambao kijamii unakubalika kuwa ni usiku sana au asubuhi sana; isipokuwa tu kama kuna dharura.

7. Chukua tahadhari ya wale walio karibu nawe wasisikie mazungumzo yako kwani waweza kupata taarifa zako za siri usizokusudia wao kuzifahamu.

8. Tuma ujumbe wenye staha na maudhui mazuri.

9. Usitunge au kusambaza ujumbe wenye maudhi au usiofaa.

10. Ukipokea ujumbe usiofaa, ufute na usiusambaze.

10.5. Unapotumia simu kupata huduma za kifedha

Simu ya kiganjani imekuwa mwezeshaji mkuu wa miama ya kifedha. Katika miaka ya hivi karibuni, kume kuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya huduma za kifedha mtandaoni. Simu ya mkononi inakuwezesha kutuma, kuhamisha au kupokea pesa mahali popote penye huduma hiyo. Hali hii imeongeza kwa kiasi kikubwa uwezo wa jamii kuweza kuzifikia na kushiriki katika huduma za kifedha kwa wingi na kwa urahisi zaidi.

Pamoja na faida nyingi zinazotokana na ukuaji huu, pia kumekuwapo ongezeko la changamoto ambazo zinaendana na matumizi ya huduma hizi. Ili kupunguza au kuondoa kabisa changamoto hizi, mtumiaji wa huduma za kifedha mtandaoni unashauriwa kuzingatia yafuatayo:

1. Usiweke kiwango kikubwa cha pesa kwenye akaunti ya fedha kwa mtandao kwa muda mrefu. Tumia huduma za Benki kutunza kiasi kikubwa cha fedha, na unapozihitaji kwa kufanya miamala, basi unaweza kuzitoa huko na kuziingiza kwenye simu kwa ajili ya matumizi yako mtandaoni.

2. Tumia namba ya siri ambayo sio rahisi mtu mwingine kukisia. Usitumie mwaka wako wa kuzaliwa au wa mtu wa karibu kama mwenza au watoto. Ni vyema kuibadili namba hiyo mara kwa mara.

3. Thibitisha na hakiki namba ya mtu unayemtumia pesa au salio kabla ya kutuma. Hapa tunasisitiza, hakikisha, hakikisha na hakikisha tena kabla ya kukamilisha muamala.

4. Usimpe mtu yeyote usiyemfahamu vizuri simu yako au kadi yako ya simu ili atumie.

5. Usitoe namba zako za siri au taarifa zako binafsi unazotumia kwa huduma za kimtandao kwa mtu yeyote, (hapa tunasisitiza usitoe kwa mtu yeyote) kwani anaweza kutozitunza vyema au yeye mwenyewe akazitumia kwa utaratibu ambao hujauridhia.

6. Ukipigiwa simu au kutumiwa ujumbe mfupi unaokuelekeza kutuma fedha, hata kama mtu anayekuagiza unamfahamu hakikisha kuwa ndiye kabla ya kutekeleza maagizo hayo. Usishinikizwe na maelekezo ya ujumbe mfupi (sms), kwa kuwa wahalifu wana njia nyingi za kulaghai. Ukiwa hujajiridhisha, mpigie simu aliyekutumia ujumbe kwa namba nyingine, au wapigie simu watu wake wa karibu kupata uhakika; vinginevyo usitekeleze maagizo hayo. Usiwe na nidhamu ya woga. Thibitisha taarifa hata kama ni kutoka kwa mwanafamilia, kwa wakubwa wako wa kazi au kwenye jamii.

7. Unapoombwa msaada au mkopo katika mazingira ya dharura, tumia njia iliyoelekezwa hapo juu ili kujiridhisha kabla ya kutoa msaada.

8. Unapopewa “dili” linalohusisha biashara yenye faida kubwa, mikopo isiyo na usumbufu, SACCOS zenye majina maarufu, unapopata taarifa ya ushindi wa donge nono katika bahati nasibu ambayo hujashiriki, kumbuka usitangulize malipo ya aina yoyote. Kumbuka utafanikiwa kwa kufanya kazi halali kwa bidii na kwa uledi na sio kwa njia za mkato.

9. Mtumiaji mwingine akikosea kukutumia fedha na akakuomba umrudishie, usitoe wala kumrudishia,



ila mwelekeze awasiliane na mtoa huduma wake ambaye atazitoa kwako na kumrudishia.

10. Iwapo umekosea kutuma fedha na kuituma kwenye akaunti/namba usiyotarajia, toa taarifa haraka kwa mtoa huduma wako na fuatilia maelekezo unayopatiwa, kisha ripoti suala hili Polisi mapema iwezekanavyo iwapo fedha hazijarudishwa.

11. Hakikisha huduma zako zote zimezuiliwa ikiwa ni pamoja na huduma za kifedha endapo utapoteza au kuibiwa simu. Kuibiwa fedha za mtandaoni baada ya kuibiwa simu au laini ya simu hutokea tu iwapo hutatoa taarifa mapema kwa mtoa huduma wako na kwa jeshi la Polisi.

12. Unapopokea maelekezo kutoka mtu anayedai ni mwakilishi wa mtoa huduma ambaye anataka uingize tarakimu kwenye simu yako au uizime simu yako kwa sababu yoyote ile atakayokueleza usifanye hivyo; badala yake nenda kwenye ofisi za mtoa huduma wako ili utekeleze maelekezo hao ukiwa ofisini kwao. Ni bora kuchelewa kuliko kupoteza. Toa taarifa kwa Mtoa huduma wako na kwa Jeshi la Polisi.

10.6. Unapotumia simu kwa biashara

Simu zimefungua fursa za ujasiriamali wa aina nyingi. Zinawezesha watu kuwa wakala wa kuuza vocha za muda wa maongezi, kufanya miamala ya kifedha, kuuza na kutengeneza simu na kuchaji simu za watumiaji wengine, kuuza na kununua bidhaa na huduma mitandaoni, n.k.

Pamoja na mambo ya kuzingatia kwa wanaotumia huduma za fedha kwa simu, wanaofanya biashara kwenye mitandao au biashara na shughuli zinazohusiana na simu wanashauriwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kujisajili kwa mtoa huduma husika kwa kutumia taarifa zako binafsi na kuepuka kutumia taarifa au vibali vya watu wengine.
2. Kuwa makini dhidi ya wahalifu. Kwa vile biashara hizi zinahusisha mzunguko mkubwa wa fedha, zinalengwa na wezi mtandaoni na wale wa kawaida.
3. Kuhakikisha kwamba simu inayotumika kwa miamala ya kifedha ni tofauti na inayotumika kwa shughuli nyingine na kuhakikisha simu hiyo haitumiwi na mtu mwingine. Vilevile waagize wahudumu wako wasipokee maagizo ya mtu mwingine kuhusiana na biashara yako. Maelekezo yote lazima yafanyike uso-kwa-uso, au kwa njia ya simu ya maongezi tu.
4. Tumia namba ya siri ambayo sio rahisi mtu mwingine kukisia. Ni hatari na uzembe kutumia mwaka wa kuzaliwa kama namba ya siri, kwani ni rahisi kukisiwa.

5. Iwapo unauza laini za simu, hakikisha unasajili wanaonunua kwa kutumia vitambulisho vyao halisi vilivyoidhinishwa na TCRA.

6. Kutokuchakachua simu au laini ya simu. Hii inahusu hasa mafundi wa simu na wamiliki wa simu husika. Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta (EPOCA) ya mwaka 2010, kifungu cha 129 kimeweka adhabu dhidi ya kuchakachua simu au laini na kifungu 135 kimeweka adhabu dhidi ya kufungulia simu ambayo imefungiwa kama sehemu ya kutekeleza mpango wa rajisi kuu ya namba tambulishi.

7. Ukipokea simu kwa ajili ya matengenezo au kwa huduma ya kuchaji, hakikisha aliyekupa ana uthibitisho wa umilki wa simu hiyo au kifaa hicho na pale inapowezekana aonyeshe risiti ya manunuzi ya kifaa husika. Weka, tumia na tunza kitabu cha kumbukumbu (rejesta) ya vifaa vyote vinavyopokelewa na kutoka. Vilevile hakikisha kuwa wahusika wanaweka sahihi zao.

10.7. Mengineyo kuhusu simu

1. Ukipoteza simu au kadi ya simu toa taarifa kwa mtoa huduma na Polisi. Kutokutoa taarifa ni kosa la jinai na adhabu ya kutokufanya hivyo ni faini, kifungu au vyote viwili.
2. Ukiokota simu au kadi ya simu toa taarifa polisi au kwa mtoa huduma. Kutumia laini ya simu au kifaa cha mawasiliano ambacho huna uhalali wa umiliki wake au ridhaa ya mmiliki ni kosa la jinai na adhabu kwa mujibu wa kifungu 126 ni faini au kifungu.



Sehemu ya pili na ya mwisho itachapishwa toleo la Aprili - Juni, 2018.



Mobile wireless boosts internet uptake

TANZANIA has 23 million internet users; mostly using mobile wireless connections in a sub sector where subscriptions to the service have tripled in six years.

The December 2017 communications statistics released by TCRA show that internet users increased from 7,520,878 in 2012 to 22,995,109 in December 2017.

The national uptake, measured against the country's population, is now 45 per cent compared to 17 per cent in 2012. There were

major leaps between 2013 and 2014 (from 9,312,272 users to 14,217,311) and between 2014 and 2015 (rising to 17,263,523).

The volume of domestic postal items declined during the period; from 22,992,828 in 2012 to 8,228,501. The fall in the number of International items was briefly arrested, and reversed, in 2015 but fell by half in 2016.

Mobile phone subscriptions increased from 27,627,156 to 40,080,954 in the period.

Fig 1: Subscriptions and Teledensity

Year	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Fixed	176,367	164,999	142,950	142,819	129,597	127,094
Mobile	27,450,789	27,442,823	34,108,851	39,665,600	40,044,186	39,953,860
Total	27,627,156	27,607,822	34,251,801	39,808,419	40,173,783	40,080,954
Penetration	61%	61%	71%	79%	80%	80%

Fig. 2: Traffic (in minutes)

Year	2012	2013	2014	2015	2016	2017
National Traffic (On & Off Net)	24,354,279,292	34,934,613,363	41,689,212,148	43,461,094,130	51,023,633,898	56,053,981,867
Traffic to International	201,827,164	198,116,642	234,080,182	219,401,125	145,972,186	99,413,092
Traffic from International	253,811,569	229,961,296	258,420,938	221,145,509	171,320,372	104,148,723
Traffic to East Africa	67,648,652	42,535,489	53,329,431	44,821,161	35,811,296	21,952,159
Traffic from East Africa	68,978,489	56,624,940	54,174,595	54,078,219	79,875,098	43,845,601
Traffic to Other International	134,178,512	155,581,153	180,750,751	174,579,964	110,160,890	77,460,933
Traffic from Other International	184,833,080	173,336,356	204,246,343	167,067,290	91,445,274	60,303,122

Fig. 3: Estimated number of internet users by technology type


Year	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Fixed Wireless	777,461	1,056,940	1,913,082	662,882	1,218,693	3,468,188
Mobile Wireless	6,031,323	7,493,823	11,320,031	16,280,943	18,014,358	19,006,223
Fixed Wired	712,095	761,508	984,198	319,698	629,474	520,698
Total	7,520,878	9,312,272	14,217,311	17,263,523	19,862,525	22,995,109
Penetration	17%	21%	29%	34%	40%	45%



Fig. 4: Domestic and International Posted Items

Year	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Domestic items	22,992,828	25,635,016	17,158,175	22,870,106	9,058,968	8,228,501
International items	8,137,969	7,225,647	5,477,634	8,389,065	3,039,816	1,892,887
Total	31,130,797	32,860,663	22,635,809	31,259,171	12,098,784	10,121,388

Fig. 5: Number of radio stations



INTERNATIONAL EVENTS CALENDAR, 2018

March

15

World Consumer Rights Day WCRD. It marks the day in 1962 when US President John Kennedy defined consumer as 'all of us' in his address to the US Congress. He outlined four consumer rights: the right to safety, to choose, to be informed and to be heard. The list of rights has since then grown. TCRA has been celebrating WCRD since 2012. This year's focus is electronic commerce with the theme: Making market places fairer.

Sept.

10-13

ITU Telecom World 2018, Durban South Africa. The event will feature an exhibition of products and services and a forum on ICTs. Experts from governments, businesses and international organizations will debate policies, strategies, business models and technologies shaping the industry. The theme is: *Better, Sooner*; underlining speedier innovations to bridge differences in access and to improve lives.

April

26

International Girls in ICT Day. The event is celebrated every fourth Thursday in April as one of the efforts to encourage girls and young women to pursue studies in science, technology, engineering and mathematics (STEM). The International Telecommunication Union (ITU) encourages ICT stakeholders to organize events involving girls and young women around the theme 'Expanding horizons, changing attitudes'.

Oct.

9

World Postal Day. It marks the creation of the Universal Postal Union in 1874. Governments, postal services providers and regulators organize activities to raise public awareness to the role of the Post in social and economic development. UPU has organized an international letter writing competition for young people in which they are required to think of a message likely to be conveyed by a letter travelling through time.

May

17

World Information Society Day. The event aims at raising awareness on ICTs. Previously it was celebrated as World Telecommunication Day. May 17 commemorates the founding of ITU in 1865. Tanzania has been celebrating the day through focussed public education campaigns including seminars, the airing of radio and television programmes and the publication of special supplements in newspapers.

Dec.

17

African Telecommunications and ICT Day. It marks the founding of the African Telecommunications Union (ATU) in 1977 as a specialised agency of the African Union for ICTs. Two reports released in 2017 by ITU and the UN Broadband Commission show the widening of the gap between the Continent and the rest of the world in access and use of the internet.



Digitizing Africa's gender divide

■ **Lokila Mosso, Tanamera Corporate (Consultants), Dar Es Salaam**
mrlokila@gmail.com

Latest reports on the global status of ICTs shows that the gap in internet use between men and women in Africa has widened. This article addresses issues around the gender digital divide in the continent.

Grappling with post-independence development challenges in the early seventies; and painfully witnessing the growing development gap between Africa and the rest of the world, Mwalimu Julius Nyerere, the Father of the Tanzanian nation urged his people to run while the rest of the world walked. (1). That rallying cry is equally relevant today in Africa as the global differences in the use of information and communications technologies (ICTs) widens.

The 2017 Measuring the Information Society Report (MISR) released by the International Telecommunication Union (ITU) shows that Africa is not only lagging behind in ICTs use, but key players in the implementation of African countries' development programmes are being left behind. Left unresolved, the digital divide may hold back development in the continent at a time when the world is experiencing a new technological revolution.

The Organization for Economic Cooperation and Development (OECD) defines digital divide as the gap between individuals, households, businesses and geographical areas at different socio-economic levels with regard both to their opportunities to access ICTs and their use of the internet for a wider variety of activities (2).

ITU defines "digital divide" as the differences in the development (and use) of information and communications technologies (ICTS) within and between countries, regions and socio-economic groupings (3).

Other definitions are the gap that exists between those people who have access to, as well as the skills to operate, ICTs and those who do not have these. (4). Access can be both physical exposure to the technology and the ability to have and use it.

According to Hamilton Mphidi (2009) digital divide is the gap that exists between people who are information literate and those who are not; it is also the gap between

people who have access to the necessary ICTs and those who do not have them. It is the disparity in access to ICTs which may result from differences in class, race, culture and geography (5).

Most definitions use the level of internet access as a factor in assessing these gaps. Internet penetration in Africa in 2017 was 21.8 per cent of the continent's population compared to 43.7 in Arab states, 65.9 in the Americas and 79.6 in Europe.

The 2017 report of the UN Broadband Commission on ICT defines access in terms of broadband, quality network speed and digital services – including health, education and financial services. The Commission was set up in 2010 by ITU and the United Nations Scientific and Cultural Organization (UNESCO) to recommend action to expand countries' broadband access as part of efforts to meet national and international development targets. Its goals were to make broadband policy universal and affordable; to connect homes to broadband, to get more people online and to achieve gender equality in access to broadband.

"The definition of the digital divide is evolving, from the original definition of coverage and being connected/un-connected, to being connected with which speed of access. We must also prevent a new digital divide between those who live in the connected world benefiting from use-cases like connected health, connected education and smart transportation, and those without access to the use-cases the Internet of Things can provide" the report says.

It identified reasons for poor access as lack of infrastructure, non-affordability of the internet, lack of skills and lack of digital content (6).

There are gaps within gaps. For example, a gap between developed and developing countries can further be expressed in terms of the different geographical regions in the latter; and differences within a region could be between urban and rural, demographics (men, women and age groups); education levels, economic and social status and levels of education and skills (7).

In a lecture on gender and the digital divide (2009), Patricia Khati cited other gaps as physical disability, access, lack of skills, cultural and behavioural attitudes with regard to technology, age, relevancy and content in terms of



language. The use of English as the main medium of communication on the web also limits accessibility by some groups (8).

Where there are imbalances between men and women in accessing ICTs, the gap is referred to as the “gender digital divide”(9) and this has been widening in Africa where only 11.6 per cent of women access the internet. “If current trends continue, 71 Per cent of female Africans might still be offline in 2020, compared with 48 per cent of men.” (10).

MISR 2017 notes the divides in terms of gender, generation (expressed in terms of age) and geographical location. Men have more access to ICTs than women; young people spend more time online than adults and there is an urban-rural divide in access.

The situation in Tanzania

A study published in August 2017 by Research Internet Africa (RIA) showed that 31 per cent of males accessed the internet compared with 27.8 per cent of females. Some 55.4 per cent of internet users were in urban areas com-

pared with 13.6 per cent in rural areas. Rankings in other categories were higher for males and urban dwellers.

Table 1: Percentage of mobile phone and internet penetration in Tanzania (individuals aged above 15)

	Mobile phone ownership	Knowing what the internet is	Internet use	Use of social media
Country-wide	57	44.6	29.8	11.9
Male	62.7	51.3	31.5	14.3
Female	52	38.7	27.8	9.8
Urban	72.6	59.2	55.4	28.9
Rural	50.5	38.6	13.6	4.8

Source: *Research Internet Africa (RIA) report, 2017.*

So what are some of the factors leading to the divides?

The 2017 Affordability report 2017 by the Alliance for Affordable internet cites social and economic barriers, illit-



Group discussion at the University of Dar Es Salaam’s College of Information Technologies.



eracy, and gender roles as among factors which keep many African women offline (11).

